# Bajeti 2024: Hatua Muhimu

### Hatua Muhimu katika Bajeti 2024: Haki na Usawa kwa Kila Kizazi

## Nyumba Nafuu Zaidi

- Mpango Mpya wa Matumizi. Ya Ardhi za Umma kwa Ajili ya Nyumba kutumia zana zote zilizopo kujenga nyumba mpya 250,000 ifikapo mwaka 2031 kwenye ardhi za umma. Hii pia inajumuisha mali za Posta ya Canada, ardhi ya Ulinzi wa Taifa, na majengo ya ofisi.
- Kujenga nyumba zaidi za kupanga au kukodisha kwa haraka, kwa kutumia ufadhili au mkopo mpya wa mkopo wa dola bilioni 15 kwa Programu ya Mkopo wa Ujenzi wa Nyumba za Kupanga, na kuongeza jumla ya programu hiyo kufikia zaidi ya nyumba mpya 131,000 ifikapo mwaka wa 2031-32.
- Kuzindua program ya Canada Inajenga, njia ya Timu Canada ya kujenga nyumba nafuu kwa tabaka la kati kwenye ardhi zisizotumika kikamilifu kote nchini. Canada Inajenga inaunganisha mikopo ya gharama nafuu kutoka serikali kuu na uwekezaji wa majimbo na mamlaka zingine ili kuongeza ujenzi wa nyumba za kupanga.
- Kutoa nyongeza ya dola milioni 400 kwa Mfuko wa Kuharakisha Ujenzi wa Nyumba wa dola bilioni 4, ambao tayari unaongeza kasi ya ujenzi wa nyumba mpya zaidi ya 750,000 katika muongo ujao shukrani kwa makubaliano 179 na manispaa, majimbo, na maeneo mengine ya nchi.
- Kuzindua Mfuko Mpya wa Udhibiti wa Nyumba za Kukodisha wa Canada wa dola bilioni 1.5 ili kulinda na kuongeza hisa ya nyumba za bei nafuu nchini Canada.
- Kutoa dola bilioni 1 kwa Mfuko wa Nyumba Nafuu ili kujenga nyumba nafuu na kuzindua Mkondo wa kudumu wa Ujenzi wa Nyumba Haraka ili kuendeleza mafanikio ya awamu tatu za awali za Mpango wa Kujenga Nyumba Haraka.
- Kuwekeza dola bilioni 1.3 zaidi kwa programu ya Kufika Nyumbani: Mkakati wa Ukosefu wa Makazi wa Canada ili kushughulikia ukosefu wa makazi na makambi.
- Kuharakisha ujenzi na uboreshaji wa miundombinu inayowezesha ujenzi wa nyumba kwa kutoa dola bilioni 6 ndani ya miaka 10 kupitia Mfuko Mpya wa Miundombinu ya Nyumba wa Canada.
- Kurahisisha utambuzi wa sifa za kielimu na uzoefu kwa wageni katika sekta ya ujenzi na kuunda fursa zaidi za ufundi stadi ili kusaidia ajira kwa wafanyakazi wa ufundi stadi ili kujenga nyumba zaidi.
- Kufanya kazi kupunguza pengo la makazi katika jamii za watu asili kwa kutangaza uwekezaji wa ziada wa dola milioni 918 ndani ya miaka mitano kwa ajili ya makazi na miundombinu ya jamii ya watu asili za Inuit na Métis.
- Kuhamasisha taasisi za elimu za Canada kujenga makazi zaidi ya wanafunzi kwa kuhakikisha zinanufaika kutokana na kuondolewa kwa kodi ya GST kwenye ujenzi wa makazi mapya ya wanafunzi.
- Kuboresha Mpango wa Wanunuzi wa Nyumba kwa kuongeza kikomo cha utoaji fedha kwenye akaunti zao kutoka dola 35,000 hadi dola 60,000, kuwezesha wanunuzi wa nyumba kwa mara ya kwanza kutumia faida za kodi ya RRSP kuokoa hadi dola 25,000 zaidi kwa ajili ya malipo ya awali, haraka.
- Kuwezesha raia na wakazi wa Canada vijana kununua nyumba zaidi kwa kukazia Mkataba wa Mikopo ya Nyumba wa Canada kuruhusu urejeshaji wa miaka 30 kwa wanunuzi wa nyumba kwa mara ya kwanza wanaonunua nyumba zilizojengwa hivi karibuni.

- Kuandaa Sheria Mpya za Haki za Wapangaji wa Canada kwa kushirikiana na serikali za majimbo na maeneo mengine kuhakikisha kuwa upangaji wa nyumba unakuwa wa haki, wazi, na unaojulikana wazi.

## Kupunguza Gharama Za Maisha Za Kila Siku

- Kuwekeza katika kusaidia kujenga sehemu zaidi za huduma za watoto ili kuongeza mfumo wa elimu ya mapema na huduma za watoto nchini Canada na kutoa huduma ya watoto kwa dola 10 kwa siku.
- Kuzindua Fidia Mpya kwa Watu Wenye Ulemavu ya Canada kuongezea kwenye fidia za majimbo na maeneo ili kuongeza ustawi wa kifedha wa zaidi ya watu 600,000 wenye ulemavu wenye umri wa kufanya kazi.
- Kuunda Mpango Mpya wa Chakula Mashuleni wa Kitaifa ili kupanua programu za chakula shuleni za majimboni na maeneo mengine ili kutoa milo bora kwa watoto zaidi 400,000 kila mwaka.
- Kuchukua hatua za kwanza kuelekea kuzindua programu ya kitaifa ya dawa za matibabu, ambayo itahakikisha gharama si kizuizi kwa wengi katika upatikanaji wa dawa za kuzuia mimba na dawa nyingi za kisukari.
- Kuendelea kusaidia kupunguza gharama za vyakula kwa kutekeleza hatua za kuimarisha ushindani katika sekta ya vyakula, kufuatilia kazi ya wafanyabiashara wa vyakula ili kusaidia kudhibiti mfumuko wa bei, na kukabiliana na kupungua kwa ukubwa wa bidhaa ili kudumisha ukubwa na ubora wa vyakula unaotarajiwa na raia na wakazi wa Canada.
- Kufanya makubwa katika kupambana na ada za ziada, kama vile ada za kutokuwa na fedha za kutosha kwenye akaunti, na kuboresha uwazi wa bei kwa ada za huduma za ziada zinazotozwa na mashirika ya ndege, ili kusaidia raia na wakazi wa Canada wa tabaka la kati kuwa na pesa zaidi mfukoni mwao.
- Kufanya marekebisho katika *Sheria ya Mawasiliano* ili kuruhusu Wacanada kuboresha, kubadili, au kusitisha huduma za intaneti ya majumbani, simu za nyumbani, na simu za mkononi bila kulipa ada zisizo za lazima.
- Kuboresha chaguzi za akaunti za benki bure na nafuu na kudhibiti ada za kutokuwa na fedha za kutosha kwenye akaunti ambazo benki zinatoza kuwa $10.
- Kuendelea kuimarisha haki ya kufanya matengenezo, ili Wacanada waweze kutengeneza vifaa vyao vilivyovunjika—kwa bei ya haki.
- Kuongeza Mfuko wa Miundombinu ya Vyakula nchini Canada kwa dola milioni 62.9 kwa miaka mitatu ili kusaidia mashirika ya kijamii nchini Canada kuwekeza katika miundombinu ya chakula katika maeneo yaliyopo, kwa kipaumbele kutolewa kwa jamii za watu asili na Weusi, pamoja na makundi mengine yanayostahili usawa.

## Ukuaji wa Uchumi kwa Kila Kizazi

- Kuhakikisha Canada inakuwa kiongozi katika uwekezaji na matumizi ya akili bandia kwa kuwekeza dola bilioni 2 kuzindua Mfuko Mpya wa Upatikanaji wa Kompyuta za AI na Mkakati wa Kompyuta ya Kisheria ya Canada ili kusaidia watafiti, biashara mpya, kupanua wigo wa nafasi kuhakikisha wanakuwa na miundombinu wanayohitaji ili waweze kuwa na uwezo wa kiushindani.

- Kuruhusu, kwa muda, biashara kufutiwa gharama za uwekezaji katika hatimiliki, vifaa vya mtandao wa data, kompyuta na vifaa vingine vya kuchakata data kuwasaidia kuongeza uzalishaji na kushindana katika uchumi wa kesho.
- Kuongeza msaada na ufadhili kwa watafiti wa shahada ya uzamili wakiwemo watafiti kutoka kwa jamii ya watu asili na jamii zao, kwa kuwaongezea viwango vya ufadhili wa msingi wa utafiti na masomo na mafunzo makazini.
- Kuongeza uwezo wa kizazi kijacho cha vyuo vikuu vya Watu Asili, vyuo vya ufundi na vyuo vingine vya juu kwa uwekezaji wad ola milioni 242.7 kwa miaka mitatu.
- Kuzindua Programu ya Dhamana ya Mkopo ya Watu Asili wa dola bilioni 5 ili kufungua upatikanaji wa mitaji kwa jamii za watu asili, kuwawezesha kushiriki katika manufaa ya miradi ya rasilimali asilia na nishati katika maeneo yao na kwa masharti yao wenyewe.
- Kutoa dola bilioni 93 za mikopo ya kodi ya uwekezaji wa kiuchumi kwa kuzingatia vipaumbele, ili kuchochea ukuaji endelevu, kuhakikisha mustakabali wa biashara za rai ana wakazi wa Canada nchini Canada, na hivyo kutengeneza ajira nzuri kwa vizazi vijavyo.
- Mikopo ya Uwekezaji ya Asilimia 10 katika Mfumo wa Ugavi wa Magari ya Umeme kwa biashara zinazowekeza katika maeneo muhimu ya mfumo wa ugavi wa magari ya umeme, kwenye gharama za majengo.
- Kusaidia miradi ya mafuta safi kwa kurekebisha Mfuko wa Mafuta Safi ili kutoa ufadhili, haraka, na kuongeza muda wa Mfuko kwa miaka minne zaidi, hadi 2029-30.